**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# TANGAZO KWA UMMA

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepokea rasimu ya Mpango wa Uendelezaji Upya eneo la Sinza kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha Sheria ya Mipangomiji Sura 355 Toleo la mwaka 2023, Mkurugenzi wa Mipangomiji anawatangazia wananchi na wadau wa maendeleo wa Manispaa ya Ubungo kuwa amepokea Rasimu ya Mpango wa Uendelezaji Upya eneo la Sinza 2026-2046.

Wadau wote mnatangaziwa kwenda katika katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Dar es salaam na Ofisi ya Kata ya Sinza kwa ajili ya kupitia rasimu hiyo na kutoa maoni na mapendekezo yenu ambayo yatakuwa sehemu ya taarifa ya uandaaji wa mpango huo. Aidha, mpango huo unapatikana katika tovuti ya Wizara www.lands.go.tz (machapisho).

Kwa mujibu wa kifungu cha 14 (2) cha Sheria hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ataratibu mijadala ya Umma (Public Hearing) kuhusu mpango huo ili kupata maoni ya wadau ndani ya kipindi cha siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Imetolewa na;

TP. Deogratias Kalimenze

**MKURUGENZI WA MIPANGOMIJI**